# Ukataji miti unavyoathiri mazingira, mifugo Pwani

Na Beatrice Shayo

WANANCHI wa Kijiji cha Chamakweza, Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani wamelalamikia ukataji miti uliokithiri na kusababisha athari kwa mifugo yao ikiwamo kufa kutokana na uharibifu wa mazingira.

Wakizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, wananchi hao walilalamikia kitendo cha ukataji miti kwa ajili ya kuchoma mkaa na kusababisha uharibifu wa mazingira na mifugo yao kukosa chakula hali inayowalazimu kuhamisha kwenda maeneo mengine kutafuta nyasi.

Jacob Samwel, mkazi wa kijiji hicho alisema ukataji wa miti umeleta athari hasa kwa mifugo kushindwa kupita kutokana na miba mingi baada ya kuchoma mkaa kukosa maji.

"Tunaathirika na hali ya jangwa zamani kulikuwa na misitu mingi na miti mikubwa kwa sasa miti hakuna kumekuwa jangwa kutokana na mazingira hayo mifugo tumeihamisha kuipeleka maeneo mengine ili iweze kupata nyasi mwaka jana mifugo mingi ilikufa," alilalamika.

Aidha, alisema mkaa unaochomwa unasafirishwa kuelekea maeneo ya mjini bila kufuata sheria na kushauri itumike nishati mbadala ikiwamo gesi ili kulinda mazingira.

"Wanatuharibia mazingira na mwisho wa siku miti itaisha tunajikuta tunapata hasara tunashauri wasishawishi watu kuja kukata miti wajitahidi kuangalia nishati nyingine kwa ajili ya kupikia ili misitu ibaki kuwa salama na jamii nyingine iweze kufurahia uwepo wa misitu," alisema.

Alisema, wanajitahidi kutunza mazingira wanapowabaini wahalifu huwakamata na kuwakataza wasiendelee kufanya uharibifu.

"Tulikuwa na mabwawa ya asili na uoto wa asili baada ya uharibifu huo wa ukataji wa miti mabwawa yamekauka hakuna kitu kwa sasa tunachangamoto tumehamisha mifugo kwenda maeneo mengine kama Mkuranga kutafuta malisho," alisema.

Naye Lengayo Koletu alisema athari ya ukataji wa miti ni ukame katika eneo hilo.

Alidai wanaofanya uharibifu huo hawachukuliwi hatua kali na kuwafanya kurudi bila woga.

Alisema wachungaji wanajisikia vibaya, hawapendezwi na hali hiyo na wakati mwingine wanapowakuta waharibifu hao porini huwakimbiza ili kuhakikisha mazingira yanalindwa.

Baadhi ya wanaofanya shughuli za ukataji wa miti, Kondo Mwaule, alisema wanafumbiwa macho kutokana na hali zao mbaya za maisha ingawa ni kweli wanafanya uharibifu wa mazingira. "Serikali iangalie ifanye jambo gani ili tupate kula na wengine wasiingie katika ukataji wa miti ikishindikana ujue wananchi wengi wataathirika," alisema.

Mwenyekiti wa kijiji cha Mbala, Lepa Mumbi, alisema tatizo hilo limekuwa ni kero kwa sababu wanakosa vivuli vya ng'ombe kupumzika.

"Pori zima linakuwa na miba na tatizo ni huo ukataji wa miti katika kijiji tunashindwa kuwakamata kuna wakati wanakuja kukata miti usiku wakijua huo muda tumelala," alisema.

Alisema mara kwa mara wamekuwa na kikao cha kitongoji na kuwaeleza marufuku ya kukata miti ndani ya eneo hilo, lakini bado wanaendelea kufanya kwa kificho.

Mumbi alisema kitongoji chao kimeathirika kwa asilimia 60 kuanzia mwaka 2018 hadi sasa kutokana na ukataji wa miti.

Aidha, aliomba wizara husika ifungue macho kuweka katazo mahususi kwa ajili ya kudhibiti biashara ya mkaa ili kulinda miti inayokatwa kienyeji.

TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

TAARIFA KWA UMMA

USAJILI WA NAMBA YA UTAMBULISHO WA MLIPAKODI (TIN) NA MATUMIZI YA MASHINE ZA KIELEKTRONIKI (EFDs) KWA WAFANYABIASHARA WOTE KATIKA ENEO LA MKOA WA KODI KARIAKOO

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwataarifu wafanyabiashara wote katika eneo la mkoa wa

MAELEKEZO> Wanaotetea nafasi zao kukaa kando kuwa[...]

# Msomera kwazidi kunoga

Na MWANDISHI WETU

SERIKALI imesema Kijiji cha Msomera kilichopo Wilaya ya Handeni mkoani Tanga, kinawekewa mipango maalumu ya kuwa shamba darasa la uchumi wa mifugo, ambapo kwa kuanzia itaweka kambi hivi karibuni ya kuhamasisha upandishaji mbegu bora za ng'ombe wa kisasa.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alisema hayo mwishoni mwa wiki alipotembelea kijijini hapo kujionea ukarabati na ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya shughuli za mifugo katika maeneo waliyohamia wafugaji kutoka Hifadhi ya Ngorongoro.

Ulega alisema nia ya serikali ni kutaka shughuli za ufugaji katika kijiji cha Msomera ziwe bora na kisasa zaidi.

"Msomera itakuwa eneo maalumu kwa uchumi wa mifugo na miundombinu inaendelea kujengwa, leo (juzi) nimeshuhudia majosho yakikarabatiwa na nimeshuhudia ng'ombe zaidi ya 1,000 wa wakazi wa kijiji cha Msomera wakiogeshwa, pia kuna kazi kubwa inaendelea ya kujengwa bwawa la kuhifadhia maji kwa ajili ya mifugo na binadamu," alisema Ulega.

Alisema kambi hiyo inatarajia kupandisha mbegu bora za ng'ombe wa kisasa zaidi ya 4,000 ili hatimaye kijiji cha Msomera hapo baadaye kiwe na ng'ombe wengi wa kisasa na bora watakaotoa maziwa mengi na nyama.

Alieleza tayari serikali imetenga zaidi ya sh. milioni 160 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha ukusanyaji maziwa katika kijiji hicho kutokana na idadi ya mifugo inayozidi kuhamia, kumilikiwa na wakazi walioondoka Ngorongoro kwa hiari.

Kwa mujibu wa Ulega, hatua hiyo ni moja ya njia ya kuvutia wawekezaji juu ya uwepo wa maziwa mengi kijijini hapo na kuvutia ujenzi wa viwanda vya kuchakata bidhaa hiyo.

Naibu Waziri huyo aliongeza, serikali inaendelea kutenga bajeti ili kuwepo kliniki ya mifugo ikiwemo mnada wa kisasa, lengo kijiji cha Msomera kiwe shamba darasa kwa wananchi hususan wanaohamia kutoka Hifadhi ya Ngorongoro wafanye ufugaji bora na kibiashara zaidi na wengine kupata fursa ya kujifunzia hapo.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Siriel Mchembe, alisema mikakati iliyopo ni kutoa elimu kwa wafugaji wote katika kijiji hicho, ambapo tayari serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imeanza mazungumzo juu ya namna ya utoaji wa elimu bora ya ufugaji wa kisasa.

Siriel alisema ndani ya muda mfupi tayari hali ya kiafya ya mifugo mbalimbali hususan ng'ombe imeanza kubadilika kutokana na uwepo wa malisho mengi na maji, hivyo kuanza kuongezeka uzalishaji wa maziwa.

Mkuu huyo wa wilaya alisisitiza ni vyema wakazi ambao bado wapo katika Hifadhi ya Ngorongoro mkoani Arusha, kutambua wanakaribishwa Msomera kwa ajili ya kuboresha maisha yao kwa kupata huduma za msingi na bora za ufugaji wa kisasa.

Aidha, alisema wananchi hao wanapaswa kuchangamkia fursa hiyo kwa sababu serikali inazidi kuweka mikakati mbalimbali ili kijiji cha Msomera kiwe mfano katika ufugaji wa kisasa.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi wa Msomera, Mwenyekiti wa kijiji hicho, Martin Oleikayo Paraketi, alishukuru serikali kwa namna inavyozidi kuboresha miundombinu ya wafugaji, ambapo Wizara ya Mifugo na Uvuvi tayari inasimamia uwepo wa maji na malisho ya mifugo.

Paraketi alieleza wamefurahishwa na ujenzi wa bwawa kubwa la kuhifadhia maji kwa ajili ya mifugo na binadamu katika kijiji hicho, linalojengwa na serikali kwa gharama ya sh. bilioni mbili na litakuwa na uwezo wa kuhifadhi maji zaidi ya lita milioni saba.

Naibu Waziri Ulega, alifanya ziara ya kikazi ya siku moja katika kijiji cha Msomera kwa lengo la kujionea ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya wafugaji yakiwemo majosho ya kuogeshea mifugo, bwawa la kuhifadhia maji ya mifugo, binadamu na maeneo ya malisho.

## FURSA NYINGINE

Hatua hiyo ni mwendelezo wa juhudi za serikali kupeleka huduma muhimu katika eneo hilo ili kuwezesha wananchi wanaohama kwa hiari kutoka Ngorongoro, waishi bila kukosa huduma muhimu.

Wiki iliyopita Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye aliwaahidi wananchi waliohamia kijijini hapo, serikali itapeleka haraka huduma za mawasiliano na habari.

Akizungumza wakati wa ziara yake katika eneo hilo la Msomera, alisema tayari mitandao ya simu imeanza kupeleka mawasiliano na kuzitaka mamlaka za redio na televisheni kuwapelekea wananchi huduma hiyo.

"Kwa kuwa waziri wa habari nimefika hapa, nawahakikishieni huduma hizo za habari zitafika hapa, watu wakitaka kuangalia televisheni waangalie na wakitaka kusikiliza redio wasikilize," alisisitiza.

Mbali na huduma hizo, serikali imewajengea wananchi wanaohamia kijijini hapo nyumba za kisasa kwa ajili ya kuhakikisha wanaishi katika makazi bora zaidi.

Aidha, serikali imeshajenga shule na kituo cha afya ili familia zinazohamia katika eneo hilo zipate fursa ya elimu na huduma za afya kwa karibu.

TUZO




**Watoka kukosa milo miwili hadi kumiliki mifugo, kujenga nyumba bora na kusomesha watoto chuo**

# Simulizi jinsi walivyotumia Sh88,000 kukimbia umaskini



Mkazi wa wilaya ya Bunda, Nyangi Mongera akionyesha baadhi ya ng'ombe anaowafuga nyumbani kwake mkoani Mara hivi karibuni. **Picha na Beldina Nyakeke**

## Sh250,000

**Faida aliyopata Mongera baada ya kuuza ng'ombe aliowanenepesha.**

> Hivi sasa nami nahesabiwa kuwa miongoni mwa matajiri hapa kijijini kwa sababu namiliki mifugo tofauti na zamani ambapo sikuwa na chochote.

Nyangi Mongera

# 'Sukuma ndani wafugaji wanaolisha mashamba'

**Na Mwandishi Maalumu, Lindi**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amemtaka Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Telack kuwakamata wafugaji wanaopiga wakulima na kulisha mifugo yao katika mashamba yenye mazao.

Ndaki alitoa maelekezo hayo wakati wa ziara yake ya kusikiliza na kutatua migogoro ya wafugaji na wakulima aliyoifanya katika wilaya za Kilwa na Liwale, mkoani Lindi juzi.

Alisema wafugaji wengi hasa wanaohamahama kutafuta malisho ndio wanaolalamikiwa na wakulima kuwa ndio chanzo cha vurugu, wanawapiga wakulima na kulisha mifugo yao kwa ubabe katika mashamba ya wakulima.

"Sasa Mkuu wa Mkoa na timu yako naomba wale wote wanaopiga na kulisha mifugo katika mashamba ya wakulima wakamatwe kuanzia leo (juzi), wawekwe ndani na wafunguliwe mashtaka ili sheria ichukue mkondo wake," alisema.

Kutokana na maelekezo hayo, Telack alichukua hatua za haraka na kuwaelekeza wakuu wa vituo vya polisi katika wilaya ya Kilwa na Liwale kuwakamata wafugaji waliowapiga wakulima na akaagiza apatiwe taarifa ya utekelezaji wa hatua hiyo haraka.

"Yupo kijana alimpiga diwani hapa wa Kata ya Kimambi na amemlipa shilingi 350,000, nasema hiyo ni dharau na haikubaliki. Nakuagiza OCD upo hapa nataka uondoke na huyo aliyemlipa diwani na wale wote wanaohusika na vitendo hivyo wakamatwe," alisisitiza.

Alisema wafugaji wote walioingia bila utaratibu mkoani humo waanze kuondoka wenyewe kabla hawajaanza kushughulikiwa kwa sababu wao ndio chanzo cha vurugu.

"Ofisa Mifugo na Mtendaji wa Kata nataka kuona wafugaji wote walioingia kinyemela wanaanza kuondoka, na wafugaji wengine mnaobaki mkiendekeza vitendo hivi nataka niwahakikishie nitawaondoa mmoja baada ya mwingine," alifafanua.

Mmoja wa wafugaji wilayani Kilwa, Kidole Hababa alisema ili vitendo hivyo viweze kukomeshwa ni muhimu serikali ikawaita wazee wa wafugaji ili washirikiane nao kwa sababu wazee hao wanawafahamu vijana wanaofanya vitendo hivyo, watatumia njia zao za kimila kuwawajibisha.

Katika hatua nyingine, Waziri Ndaki aliwataka wafugaji kushiriki katika kusajili mifugo yao huku akiwahimiza kuanza kumiliki maeneo yao ya kufugia akiamini kuwa wakifanya hivyo itasaidia kupunguza migogoro baina yao na wakulima kwa kiasi kikubwa.

CamScanner

**4,924>>Ngo'ombe waliopatiwa chanjo ya ugonjwa wa vipele**

# Ngo'mbe wapatiwa chanjo kudhibiti ugonjwa wa vipele

**Na JUMBE ISMAILLY**, Hanang

HALMASHAURI ya Wilaya ya Hanang, mkoani Manyara, imetoa chanjo ya ugonjwa wa vipele vya ngozi kwa ng'ombe 4,924 kuanzia mwaka 2019 hadi mwaka juzi.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Elizabeth Lusingu, alibainisha hayo mbele ya [illegible] na kufafanua ng'ombe 2,276 waliopatiwa chanjo hiyo mwaka 2019 na 2,648 waliopatiwa mwaka juzi, huku mwaka jana hakuna waliopatiwa huduma hiyo.

Alieleza bayana ng'ombe 4,924 waliopatiwa chanjo hiyo ndani ya miaka mitatu ni kati ya 389,746 waliotarajiwa kupatiwa huduma hiyo katika kipindi hicho.

"Jumla ya ng'ombe 389,746 walitarajiwa kupatiwa chanjo ya ugonjwa wa vipele vya ngozi, lakini kwa sababu mbalimbali lengo halikufikiwa, badala yake tulichanja 4,924," alisema.

Akifafanua zaidi malengo waliyojiwekea ya chanjo hiyo kipindi cha miaka mitatu, mkurugenzi huyo alisema kwa mwaka 2019 hadi 2020 walitarajia kuchanja ng'ombe 124,345 kila mwaka.

Kuhusu changamoto katika chanjo hiyo, alisema baadhi yao walitegemea kupatiwa bure, wengine walihamisha mifugo wakati wa chanjo na uhaba wa vitendea kazi kwa wataalamu kupeleka chanjo maeneo ya vijijini.

Naye, Ofisa Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang, Kenneth Ngadada, alibainisha endapo mifugo haitapatiwa chanjo ya kukinga na ugonjwa huo, kuna madhara yanayoweza kujitokeza.

Aliyataja madhara hayo ni kutopatikana maziwa ya mifugo ya [illegible] na vifo endapo ugonjwa huo utatokea.

Kwa mujibu wa takwimu ya halmashauri hiyo, ina ng'ombe 282,111, mbuzi 192,300, kondoo 102,751, punda 17,501, nguruwe 10,019, mbwa 17,501, paka 9,927, sungura 9,641, kuku 279,922, kanga 594 na bata 155,797, hivyo kufanya idadi ya mifugo kufikia 1,078,064.

MIFUGO



[illegible]

## SUMA JKT kujikita zaidi kilimo cha umwagiliaji

KUFUATIA maadhimisho ya miaka 41 tangu kuanzishwa kwa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (Suma JKT), jeshi hilo limeamua kuendelea kujikita katika kilimo cha umwagiliaji badala ya kutegemea mvua.

Umesema ni kufikia lengo hilo, limeanza mchakato wa kilimo hicho katika shamba lake lenye ekari 3,000 lililoko eneo la Mbigiri(?), mkoani Morogoro.

Kaimu Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Suma JKT, Kanali Shija Lupi, alisema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, katika Maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF).

"Kilimo cha umwagiliaji ndicho chenye tija zaidi badala ya kutegemea

> Kilimo cha umwagiliaji ndicho chenye tija zaidi badala ya kutegemea cha kusubiria mvua...Kupitia kilimo hiki tutalima mara nyingi kwa mwaka mmoja.
>
> Kaimu Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Suma JKT, Kanali Shija Lupi

cha kusubiria mvua. Kupitia kilimo hiki tutalima mara nyingi kwa mwaka mmoja na hivi sasa tunafanyia majaribio(?) mashamba yetu," alisema.

Akizungumzia miaka 41 ya kuanzishwa kwa shirika hilo, Kanali Lupi alisema Suma JKT imeendesha shughuli zake za sekta za ujenzi, kilimo na ufugaji ambazo zimeleta na tija na kuinua kipato cha mwananchi mmoja mmoja.

Akiongelea kupitia sekta ya kilimo, ndani ya miaka hiyo, shirika hilo limekuwa likijishughulisha na mradi wa kuuza matrekta ya kisasa yaliyoleta mapinduzi kwa wakulima kwa kuzalisha mazao yao kwa wingi kwa kutumia zana bora.

Katika sekta ya ufugaji, alisema wanafuga samaki kwa kisasa zaidi, hali inayosaidia kukuza pato la taifa na la mtu mmoja mmoja na wanawajengea uwezo wananchi ufugaji bora wa samaki.



Mkuu wa Idara ya Biashara wa NMB, Alex Mgeni, akitoa maelezo ya namna ya kupata mkopo kupitia huduma ya Mahiko Fasta kwa wafanyabiashara wakubwa kwenye mtandao thabiti kwa ukuaji endelevu wa biashara, ili nao wakawaeleze wafanyakazi wao jinsi ya kukopa kupitia simu zao. Semina hiyo ilifanyika katika Hoteli ya Malaika jijini Mwanza. (Picha na Mpiga Picha Maalumu)

# Kanda ya Ziwa wahimizwa kuchukua mikopo ya uvuvi

**Na Mwandishi Wetu**

WANANCHI wa Kanda ya ziwa, wameendelea kuhamasishwa kuchangamkia mikopo mbalimbali ikiwemo ya boti za uvuvi ili kuchangia ukuaji wa uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla, kupitia sekta ya uvuvi.

Mkuu wa Idara ya Biashara wa Benki hiyo, Alex Mgeni wa Benki ya NMB, alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano wa mtandao thabiti kwa ukuaji endelevu wa biashara.

Mkutano huo uliandaliwa na NMB na kuwakutanisha wafanyabiashara wakubwa wa mkoa wa Mwanza, kujadili masuala mbalimbali, ikiwemo upatikanaji rahisi wa mikopo ya benki hiyo kwa ustawi wa biashara zao.

"Tumeshatoa mikopo ya aina hii Zanzibar kwa ajili ya uvuvi na utalii. Boti zinatumika kubeba watalii," alisema na kuongeza kwamba kwa Kanda ya Ziwa, Benki italeta mikopo ya boti za uvuvi, lakini endapo kuna mahitaji pia ya boti za utalii, NMB itaweza kufanya hivyo.

Alisema rasilimali na mtaji wa Benki vinakuwa kila mwaka kiasi kwamba sasa ina uwezo wa kukopesha hadi kiasi cha sh. bilioni 250 kwa mtu mmoja. Kwa mujibu wa mgeni, kwa sasa rasilimali za Benki ni sh. trilioni 8.7 na amana za wateja sh. trilioni 6.6.

Washiriki wa mkutano huo, akiwemo Mshauri wa Masuala ya kodi katika kampuni ya Onduchi Associate, Nicas Nibengo alichangia kwamba wafanyabiashara wote wanafahamu kulipa kodi bila shuruti ni wajibu wao, lakini serikali iendelee kuweka mazingira rafiki.

Alishauri kushuka kwa kiwango cha kodi ya ongezeko la thamani (VAT), kutoka asilimia 18 za sasa hadi 15, kama ilivyo kwa nchi ya Kenya ili wawekezaji wa Tanzania waweze kuhimili ushindani katika sekta ya biashara.

"Kwa sasa mshindani wetu mkubwa ni Kenya. Kiwango cha VAT nchini Uganda ambacho ni asilimia 16 hakitusumbui sana," alisema.

Alitoa pongezi kwa muandaaji wa mkutano huo ambao ulitoa fursa kwa wafanyabiashara hao kujifunza mambo mengi kwa ustawi wa biashara zao, ikiwemo utoaji mikopo ya vifaa vya kufanyia kazi, utunzaji kumbukumbu za biashara pamoja na ulipaji bora wa kodi.

Akifungua mkutano huo, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza (RC), Mhandisi Robert Gabriel, aliwakaribisha wafanyabiashara hao kuwekeza hasa katika sekta ya utalii, uvuvi na kilimo, akasema.

Tayari serikali imeandaa maeneo ya ufugaji wa samaki wa vizimba katika Ziwa Victoria na miundombinu yote muhimu imeshawekwa.

"Tunasubiri wawekezaji tu. Lakini pia tunaweza kuwekeza kwenye kilimo cha kimkakati kwani ardhi ya Mwanza inastawisha kila aina ya mazao," alisema na kuongeza kwamba